

MARIAM, YESU NA UKRISTO

KWA

MTAZAMO WA KIISLAM

(Mary, Jesus and Christianity: An Islamic Perspective)

Kimeandikwa na:
Mohammad Shomali

Kimetarjumiwa na:
Ramadhani Kanju Shemahimbo

©Haki ya kunakili imehifadhiwa na:

AL-ITRAH FOUNDATION

ISBN: 978 - 9987 - 512 -30 - 0

Kimeandikwa na:
Mohammad Ali Shomali

Kimetarjumiwa na:
Ramadhani Kanju Shemahimbo

Kimepangwa katika Kompyuta na:
Hajat Pili Rajab

Toleo la kwanza: Augasti, 2008
Nakala: 1000

Kimetolewa na kuchapishwa na:
Alitrah Foundation
P.O. Box 19701 Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 2110640
Simu/Fax: +255 22 2127555
Email: alitrah@raha.com
Website: www.alitrah.org
Online: www.alitrah.info

YALIYOMO

Mariam Yesu na Ukristo mtazamo wa Kiislamu.....	2
Mariam (Mary).....	5
Yesu (Isa).....	11
Uhusiano wa Waislamu na Wakristo.....	13
Bibliografia.....	23

MARIAM, YESU NA UKRISTO MTAZAMO WA KIISLAMU

DIBAJI

Uislam, kama dini nyingine za Ki-Abraham unaamini katika upweke wa Mungu. Mungu ni Mmoja, Yeye hana mshirika na hakuna chochote kina-chofanana naye.

Mungu yu Pekee; hana viungo wala sehemu. Yeye ndiye Muumba pekee na mlengwa (mshabahiwa pekee wa) pekee wa kweli wa ibada. Matokeo ya dhahiri ya dhana hii juu ya Mungu ni kwamba ulimwengu ni lazima uwe na mpangilio mzuri na msimamo. Hakika, moja ya ishara za upweke wa Mungu ni ukweli kwamba hakuna mgawanyiko au mtengano na pengo katika sehemu yoyote ile ya ulimwengu. Qur'ani inasema:

“Laiti kama wangelikuwemo humo mbingu na ardhini waungu wengine mbali na Mwenyezi Mungu, zote zingeharibika.”(21:22)

Upatanifu na msimamo huu katika maumbile ya ki-ungu unaendelea mpaka kwenye funuo (wahyi) zake. Ujumbe wa kiungu uliowasilishwa kwa watu kuititia Mitume Wake unapaswa kuwa na upatanifu pia. Kama ufunuo huu unafunuliwa na Mungu huyo huyo kwa wapokezi wake (wanadamu) ambao wana asili moja na mahitaji ya msingi ili kuwaonyeshaa njia ya kuelekea kwenye ukamilifu bora kiasi iwezekanavyo na furaha, lazima uwe unafanana katika asili na sawa sawa katika dhati yake. Bila shaka, kutegemeana na hali zinazotofautiana, na hali ya mambo, baadhi ya maelezo yanaweza kubadilika.

Hivyo waislam wanaamini katika upatanifu wa wahyi zote na ubashiri wa kinabii. Wanathibitisha na kuamini mitume wote na wanawachukulia wale wote wanaoamini katika Mungu kuwa ni watu wa jamii moja ya imani.

Upweke wa Mungu unaonekana katika umoja wa ufunuo Wake na lazima ufanane katika umoja wa wote wale wanaoamini Mungu. Uislam umeleta umoja na pia mshikamano kwa wale ambao waliteseka kwa kiasi kikubwa kutokana na uadui na ukatili (3:103). Kitendo hiki cha kuunganisha watu kinatukuzwa sana kama kitendo kitakatifu (8:63). Kinyume chake, kitendo cha watu kama Firauni kilikuwa ni cha kuwagawanisha watu (28:4). Qur'ani inawaonya waumini kwamba endapo wataanza kuzozana wenyewe kwa wenyewe watajidhoofisha na kwa hiyo wao watashindwa (8:46). Kwa kweli wito wa umoja haukuwekewa mipaka kwa Waislam tu. Qur'ani tukufu inawaita watu wote wa dini kama vile Wakristo na Wayahudi kuunganisha nguvu na jitihada zao za kumakinika katika hoja zao zinazokubalika kwa wote (3:64).

Moja ya njia bora ya kufanikisha umoja huu na udugu ni kufahamiana, kila mmoja kumfahamu mwenzie, kuzishinda chuki zao za kihistoria zinazozuia kule kulielewa lengo baina yao na kujenga ushirikiano wa pamoja wa kawaida. Kwa mujibu wa kile alichosema Imam Ali (a.s): "Watu ni maadui wa kile wasichokijua."

Kwa msimamo huu, insha inayofuata iliandikwa. Illichapishwa kwanza katika kitabu "*Catholics and Shi'ah in Dialogue: Studies in Theology and Spirituality*", kilichohaririwa na Anthony O'Mahony, Wulstan Peterburs na Mohammad Ali Shomali (London: Melisende, 2004) na kwa sasa hivi, pamoja na mabadiliko madogo madogo, kitachapishwa tena na taasisi ya masomo ya Kiislam - Institute of Islamic Studies, iliyoshirikishwa na Islamic Centre of England - Kituo cha Kiislam - Uingereza. Inategemewa kwamba chapisho hili linaweza kutumika kama njia ya unyenyekevu ya kuwaleta karibu zaidi wafuasi wa dini kuu mbili za dunia: Uislam na Ukristo, ambao wanaunda nusu ya idadi ya watu duniani. Hapa juhud zimefanyika kuwasilisha picha fupi na kamilifu ya Mariam na Yesu ndani ya Uislam na kuelezea ni kwa nini Waislam na Wakristo wapaswe kuingia kwenye mjadala wa kweli, halisi na wenye manufaa.

Tutegemee na kuomba kwamba siku hadi siku hisia hii ya umoja na

mshikamano iwe inaongezeka na inasaidia kufanikisha lengo la dini:
Kumjua Mungu, na kusimamisha jamii ya haki na usawa katika dunia hii.

Mohammad Ali Shomali
Novemba, 2007/ Shawwal 1428





NENO LA MCHAPISHAJI

Kitabu kilichoko mikononi mwako ni tarjuma ya kitabu cha Kiingereza kwa jina la, *Mary, Jesus and Christianity: An Islamic Perspective*. Sisi tumekiita, *Mariamu, Yesu na Ukristo: Kwa Mtazamo wa Kiislamu*.

Kitabu hiki ni matokea ya kazi ya kielimu iliyofanywa na mwanachuoni wa Kiislamu aitwaye Mohammad Ali Shomali

Waislamu wanaamini kwamba idadi ya Mitume wote waliotumwa na Mwenyezi Mungu ni zaidi ya 124,000 - wa kwanza wao ni Adam (a.s.) na wa mwisho wao ni Muhammad (s.a.w.). Miongoni mwa Mitume hao, wako ambao Mwenyezi Mungu amewatukuza zaidi kuliko wengine, akiwemo Isa (Yesu) bin Maryam (Mariamu): “*Mitume hao tumewafadhilisha baadh-i yao zaidi kuliko wengine. Miongoni mwao yuko ambaye Mwenyezi Mungu alisema naye; na wengine akawapandisha vyeo, na tukampa Isa mwana wa Maryam dalili zilizo wazi na tukamtia nguvu kwa roho takatifu....*” (Qur’ani 2:253)



Ingawa Mitume wote kazi yao ilikuwa ni kufikisha ujumbe kwa wanadamu, lakini wao ni kama walimu ambao kazi yao ni kufundisha, isipokuwa tu hutofautiana katika ufundishaji, k.v. wako wanaofundisha shule za msingi ambao hawalingani na wanaofundisha shule za sekondari na ambao hawalingani na wanaofundisha katika vyuo vikuu. Lakini pamoja na kutolingana huko, wote kazi yao ni kufundisha - ni walimu: “*Mtume ameamin yaliyoteremshwa kwake kutoka kwa Mola wake, na wenye kuamini, wote wamemwamini Mwenyeze Mungu, na Malaika Wake, na Vitabu Vyake, na Mitume Yake, (husema): ‘Hatutofautishi baina ya Mitume Wake’ ...*” (Qur'an 2: 285).



Kitabu hiki ni chenye manufaa sana, kwani kitawaleta karibu na kujuana wafuasi wa dini hizi mbili - Uislamu na Ukristo. Kutokana na ukweli huu, Taasisi yetu ya Al-Itrah Foundation imeamua kuchapisha kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili kwa madhumuni yake yaleyale ya kuwashudumia Waislamu, hususan wazungumzaji wa Kiswahili, ili kuongeza ujuzi wao katika masuala ya kidini na kijamii.

Tunamshukuru ndugu yetu, Ramadhani Kanju Shemahimbo kwa kukubali jukumu hili la kukitarjumi kitabu hiki. Vilevile tunawashukuru wale wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwake.

Mchapishaji:
Al-Itrah Foundation
S. L. P. 19701
Dar-es-Salaam, Tanzania.



Mariam, Yesu na Ukristo kwa Mtazamo wa Kiislam

Mariam, Yesu na Ukristo Mtazamo wa Kiislamu

Ni vigumu sana kuandika kuhusu watu ambao kwao mtu kwa binafsi amejiambatanisha nao. Kwangu mimi kama mtu niliyelelewa katika utamaduni wa Kiislam, Mariam na Yesu wakati wote wamekuwa kati ya wale watu mashujaa ambao maisha yao yanapaswa kuchukuliwa kama mfano muhimu sana na wa kuigwa. Ninakumbuka kwamba wakati nikiwa ninaishi Tehrani, kama kijana, nilikuwa nikihudhuria msikiti wa hapo nyumbani kwa ajili ya swala za jamaa. Kwa kawaida ndani ya misikiti, baada ya swala ya jamaa, mtu mmoja husoma baadhi ya aya za Qur'ani au du'a fulani. Kama ilivyokokotezwa katika baadhi ya Hadithi, katika msikiti wetu zile aya mbili za mwisho za sura ya pili ya Qur'ani zilikuwa zikisomwa mara kwa mara na kwa masiku na masiku nilikuwa nikizisikiliza na kuzitafakari juu yake. Ile ya kwanza yake inasomeka kama ifutavyo:

“Mtume ameamini yaliyoteremshwa kwake kutoka kwa Mola wake, na wenye kuamini, wote wamemuanini Mwenyeezi Mungu, na Malaika Wake, na Vitabu Vyake, na Mitume Yake, (husema): Hatutofautishi baina ya Mitume yake, na husema: Tumesikia na tumetii tunaomba msamaha Wako, Mola wetu na marejeo ni Kwako. (2:285)”

Aya hii, kama aya nyingine nyingi za Qur'ani, inaweka msisitizo mkubwa katika ulinganifu wa mitume, vitabu au maandiko yao, na ujumbe wa kila mmoja wao. Inakufanya ufikiri kwamba wewe ni wa jumuiya kubwa ya imani ikiwa ni pamoja na waumini wote mwote katika historia ya mwanadamu ambaye amefuata njia hiyo hiyo, kwa hiyo, kwangu mimi, watetezi wote wa njia hii wanaheshimiwa sana. Miongoni mwao, baadhi yao wamejipambanua sana. Yesu alikuwa mmoja kati ya wale Mitume

Mariam, Yesu na Ukristo kwa Mtazamo wa Kiislam

watano mashuhuri.¹ Mariam alichaguliwa juu ya wanawake wote wa dunia (3:42) na kutambulishwa kama mfano wa wale wanaoamini (66:12). Katika (gazeti) makala hili kwanza nitajaribu kuelezea kwa ufupi baadhi ya sura za watu kama Mariam na Yesu kwa mtazamo wa kiislam na halafu nitarejeza kwenye mahusiano ya Muislam na Mkristo.

Pengine zaidi kuliko mama na mtoto wengine, Mariam na Yesu walikuwa wamehusiana na kuungana pamoja. Inavutia sana kwamba katika Surah ya 21 “Surat-Anbiyaa.” Qur’ani inataja majina ya baadhi ya Mitume, lakini pale inapofika kwa Yesu, inazungumza kuhusu Mariam, na kupitia yeye kuhusu Yesu na Inasema: “**Na (Mkumbuke mwanamke) yule aliyejilinda tupu yake, na tukampulizia roho yetu na tukamfanya yeye na mwanawe kuwa muujiza kwa walimwengu.**” (21:91)

Qur’ani hapa inamtaja Mariam na mwanawe kama: “Muujiza kwa walimwengu.”² Kwa nini? Tafsiri yenyewe ufanuzi ya aya hii inatolewa na Allamah Tabatabai ambaye anashikilia kwamba huo muujiza hapa ni kule

¹ Kwa mfano, tazama *Usul al-Kafi*, Juz.1, uk. 175, Hadithi namba 3. mahali pengine nimeandika hivi: “Qur’ani inawataja mitume ishirini na tano na inaeleza kwamba walikuwepo wengine zaidi. (40:78) kwa kupitia dalili za hadithi, waislam wanaamini kwamba walikuwepo manabii 124,000. Mionganoni mwa wale waliotajwa kwenye Qur’ani ni Adam, Nuh, Ibrahim, Isma’il, Is’haq, Lut, Yaqub, Yusuph Ayyub, Musa, Harun, Hizqil, Daudi, Suleiman, Yunus, Zakariah, Yahya (Yohana Mbatzaji) Isa na Muhammad. Mionganoni mwao, Nuh, Ibrahim Musa, Isa na Muhammad walikuwa na ujumbe kwa watu wengi (kama sio wote) na walileta kanuni mpya za Sheria. Wao hawa wanaitwa ‘Ulu al-Adhm’ kwa maana ya wale wenye dhamira kuu.” (M.A Shomali (2003), *Discovering Shi'i Islam* (Qum: Jami’at al-Zahra), uk. 43).

² Hii haina maana kwamba kutoka kwenye mtazamo mwengine kila mmoja wao peke yake hawezi kuchukuliwa kama alama ya Mungu, kwa mfano, katika aya ya 19:21, Mungu anasema kwamba yeye anataka kumteua mwana wa Mariam kama dalili kwa wanadamu na Rehma.

Mariam, Yesu na Ukristo kwa Mtazamo wa Kiislam

kuzaliwa kwa Yesu kutoptana na Mariam. Anaongeza kuwa kile kitendo cha kwamba Mariam anatajwa wa kwanza mwanzoni pamoja na Mitume hao (ingawaje yeye hakuwa Mtume) halafu yeye na mwanawe wanatambulishwa kama “muujiza” ni heshima kubwa sana kwa Mariam.”³

Nadhani ni kweli kwamba mazazi haya yalikuwa maalum sana na hasa inaweza kuchukuliwa kama “muujiza” wa Mungu. Kama tujuavyo, Qur’ani inathibitisha uzazi wa kibikira wa Yesu kama ifuatavyo:“.....Ewe Mariam! Hakika Mwenyezi Mungu anakupa habari njema za neno litokalo Kwake; jina lake ni Masihi Isa mwana wa Mariam, mwenye heshima ulinwenguni na akhera, na ni miongoni mwa wenyewe kukurubishwa mbele ya Mwenyezi Mungu. Atasema na watu katika uchanga wake na utu uzima, na atakuwa katika watu wema. Akasema (Mariam), Mola wangu! Nitapataje mtoto na hali hajanigusa mwanaume yoyote? Akasema: Hivyo ndivyo; Mwenyezi Mungu huumba atakavyo, anapokusudia jambo huliambia kuwa “nalo huwa.” (3:45-47)

Kwa hakika Yesu alizaliwa kimuujiza kupitia kwenye nguvu ile ile ambayo ilimleta Adam kwenye uhai bila ya kuwa na baba.“**Hakika mfano wa Isa mbele ya Mwenyezi Mungu ni kama mfano wa Adam, alimuumba kwa udongo, kisha akamwambia kuwa, basi akawa.**” (3:59)

Hata hivyo ile aya (21:91) inaelekea kurejelea kwenye jambo jingine zaidi, kwa vile inaashiria kwamba Mungu “alimfanya yeye na mwanawe kuwa muujiza” na sio ule uzazi tu. Inavutia kwamba mahali pengine tena Qur’ani inamtaja Mariam na Yesu kama “Muujiza”

“Na tulimfanya mwana wa Mariam na mama yake kuwa Muujiza, na tukawapa kimbilio mahali palipoinuka penye utulivu na chemchem.”
(23:50)

³ Tazama: *al-Mizan fi Tafsir al-Qur'an*, Juz.14 (Qurm: Isma'iliyan, 1972), uk.317

Mariam, Yesu na Ukristo kwa Mtazamo wa Kiislam

Mariam na Yesu walikwua karibu sana na kila mmoja wao. Haikuwa ni jambo la utukizi au la kubahatisha (sadifa) kwamba Mariam angeweza kupata mtoto kama Yesu kwa hiyo hebu tuone Mariam alikuwa ni nani:

MARIAM (MARY)

Mariam ndiye mwanamke pekee anayetajwa kwa jina ndani ya Qur'ani. Kuna Surah nzima kabisa ndani ya Qur'ani iliyopewa jina la "Mariam." Yeye ametajwa mara 34 ndani ya Qur'ani, zaidi kabisa kuliko ndani ya Biblia. Kuzaliwa kwa Mariam kulikuwa maalum kabisa. Wazazi wake yaani Imran (Joachim katika simulizi za Kikristo) na Hannah walikuwa wazee na hawakuwa na mtoto kwa muda mrefu baada ya ndoa yao. Mwenyezi Mungu alimfunulia Imran kwamba watapewa mtoto wa kiume aliyebarikiwa ambaye ataweza kuwaponya wagonjwa, kufufua wafu na (atakuwa) Nabii wa kabila la Israili. Imran alimjulisha Hannah kuhusu mtoto huyu na kwa hiyo kila mmoja alikuwa anategemea mtoto, wa kiume.⁴ Wakati Hannah alipokuwa mjamzito, alitaka kumfanya mwanawе kuwa mfuasi maalum wa Mwenyezi Mungu.⁵ Hebu tuifuatilie simulizi hii kutoka ndani ya Qur'ani:**"Wakati aliposema mke wa Imran: Mola wangu! Hakika nimeweka nadhiri kwako, aliyomo tumboni mwangu kuwa waqfu, basi nikubalie, bila shaka wewe ndiye Mwenye kusikia mwenye kujuja yote.**

"Basi alipomzaa akasema: Mola wangu! Hakika nimemzaa mwanamke, na Mwenyezi Mungu anamjua sana aliyemzaa, na mwanaume sio mwanamke. Na mimi nimemwita Mariam, nami nam-linda kwa nguvu Zake, (Yeye) na kizazi chake (awalinde) na shetani

⁴ Ayatullah Nasir Makarim Shirazi, *Qissiba-ye Qur'an* (Tehran: Dar al-Kutub al-Islamiyyah, 2001), uk. 323

⁵ Neno la Kiarabu ambalo limetumika kwenye Qur'ani ni 'Muharrar,' ambalo lina maana ya aliyetengwa, huru (kutukana na mambo ya kidunia na hususan aliyejitoa kumtumikia Mungu).

Mariam, Yesu na Ukristo kwa Mtazamo wa Kiislam

mwenye kufukuzwa. "Basi Mola wake akamkubali kwa mapokezi mazuri, na akamlea malezi mema, na akampa Zakaria kumlea. Na Zakaria kila aingiapo kwake (Mariam) chumbani, hukuta vyakula pamoja naye akasema: Ewe Mariam umevipata wapi hivi? Akasema: Vinatoka kwa Mwenyezi Mungu, hakika Mwenyezi Mungu humruzuku amtakaye bila ya hesabu."⁶ (3:35-37)

Kwangu mimi moja ya nukta za kuvutia katika hadithi hii ni kwamba, Imran na Hannah waliambiwa kwamba watapata mtoto wa kiume, yule Masihi. Badala yake walimpata Mariam, mama wa mtoto huyo. Ni kweli kwamba kijana wa binti yake mtu wakati mwingine kuchukuliwa kama ni kijana wake wenyewe, lakini nafikiri hii ni ishara nytingine ya ule uhusiano wa Mariam na Yesu kana kwamba Mariam ndio mwanzo wa Yesu. Inavutia vile vile kwamba kwa mshangao wa wengi, kama sio wote, ahadi ya Hannah ya kumfanya mwanawewe kuwa ni mtumishi mwaminifu wa Mungu, hiyo ilikubaliwa na Mwenyezi Mungu ndani ya Mariam na kwa mara ya kwanza msichana aliruhusiwa kukaa na kuishi ndani ya Hekalu.⁷

Sio tu kwamba Mariam alizaliwa kwenye nyumba au familia ya kiuchamungu, bali pia alilelewa chini ya Uangalizi wa Nabii Zakariah kat-

⁶ Ilikuwa ni kauli hii ya Mariam ambayo ilimtia msukumo Mzee Zakariah kumuomba Mungu ili kupata mtoto, Mara tu baada ya aya hizo hapo juu, Qur'ani inasema: "Palepale Zakariah akamuomba Mola Wake, akasema: Mola Wangu! Unipatie kutoka Kwako kizazi kizuri, hakika wewe ndiye Mwenye kusikia maombi. Mara Malaika wakamwita naye amesimama akiswali chumbani kwamba: Mwenyezi Mungu anakupa habari njema za Yahya, atakayekuwa mwenye kusadikisha neno litokalo kwa Mungu, na Bwana, na Mtawa, na Nabii mionganoni mwa watu wema. Akasema: Mola wangu! Nitapataje mtoto na utu uzima umenifikia, na mke wangu ni tasa? Akasema: Hivyo ndivyo hivyo, Mwenyezi Mungu hufanya atakavyo." (3:38-40)

⁷ Baadhi ya Wafasiri wa Qur'ani wamesema kwamba dalili ya kukubali kwa Mwenyezi Mungu huyu Mariam ilikuwa kwamba aliwekwa huru kutokana na hedhi ili asilazimike kutoka mle Hekaluni. Imesimuliwa katika *al-Makarim Shirazi*, uk. 324

Mariam, Yesu na Ukristo kwa Mtazamo wa Kiislam

ka sehemu safi na takatifu kama lile Hekalu.⁸ Yeye mwenyewe binafsi ali-jarbu kupata utakaso na uchamungu kwa kumtumikia Mungu kwa moyo wake wote. Katika yanayofuata nitajaribu kurejea haraka haraka kwenye baadhi ya sifa za Mariam au mafanikio ambayo yamemfanya yeye kuwa mfano:

Ubikra⁹

Utii¹⁰

Uaminifu¹¹

Kutakaswa na Mungu¹²

Kuchaguliwa na Mungu juu ya Wanawake wote¹³

Kusemeshwa na Malaika¹⁴

⁸ Kwa mujibu wa simulizi za Kiislam, Imran alikuwa amefariki kabla ya kuzaliwa kwa Mariam.

⁹ Kwa nyongeza ya aya ya 21:91 ambayo imetajwa hapo kabla, mtu anaweza kurejea kwenye aya zifuatizo: “Na Mwenyezi Mungu anapiga mfano wa walioamini kwa mkewe Firauni aliposema: ‘Ewe Mola wangu! Nijengee nyumba Peponi karibu Yako, na unioke na Firauni na matendo yake, na unioke na watu madhalimu. Na Mariam binti Imrani aliyejilinda tupu yake, na tukampulizia humo roho yetu, na akayasadikisha maneno ya Mola wake, na Vitabu vyake, na yeye alikuwa mionganoni mwa wanyenyekevu.’” (66:11-12)

¹⁰ “Yeye (Mariam)..... alikuwa mionganoni mwa wanyenyekevu.” (66:12)

¹¹ “Yeye Mariam alishuhudia kwa uaminifu juu ya maneno ya Mola wake na Vitabu vyake.” (*Ibid*)

“Masih bin Mariam hakuwa chochote ila ni Mtume, na bila shaka mitume wengi wamepita kabla yake. Na mama yake alikuwa mkweli, wote walikuwa wakila chakula. Tazama jinsi tunavyowabainishia dalili mbali mbali, kisha tazama vile jinsi wanavyoyeuzwa.(5:75).

¹² “Kumbuka” Malaika aliposema: Ewe Mariam! Hakika Mwenyezi Mungu amekuchagua na amekutakasa, na amekuchagua kuliko wanawake wote wa ulimwengu. (3:42)

¹³ *Ibid.*

¹⁴ *Ibid*

Mariam, Yesu na Ukristo kwa Mtazamo wa Kiislam

Kupata chakula kutoka kwa Mungu¹⁵

Kupashwa habari ya kumzaa Yesu¹⁶

15 “Na kila Zakaria aingiapo kwake chumbani humkuta pamoja na vyakula naye akasema: Ewe Mariam! umevipata wapi hivi? Akasema: ‘Vyatoka kwa Mwenyezi Mungu, hakika Mwenyezi Mungu kumruzuku amtakaye bila hesabu.’” (3:37)

16 Tayari tumekwishataja baadhi ya aya za Qur’ani tukufu kuhusu kule kubashirisha kwa Isa (Yesu). Hapa ningependa kurejea kwenye maelezo ya kina zaidi kuhusu kuzaliwa kwake kutoka kwenye *Surat-Mariam*:“Na Mtaje Mariam kitabuni, alipojitenga na jamaa zake, (akaenda mahali upande wa mashariki, na akaweka pazia kujikinga nao, kisha tukampeleka Malaika Wetu kwake, aliyejitalibusha katika sura ya mtu kamili. (Mariam) akasema: Hakika mimi najikinga kwa Mwingi wa rehema aniepushe nave, ikiwa unamuogopa Mungu. (Malaika) akasema: hakika mimi ni mjambe wa Mola Wako, ili nikupe mwana mtakatifu. Akasema: ninawezaje kupata mtoto na hali hajanigusa mwanaume yejote, wala mimi sio asherati? (Malaika) Akasema: hibyo ndio itakavyokuwa, asema Mola Wako: Haya ni rahisi Kwangu. Na ili tumfanye muujiza kwa watu na rehma itokayo Kwetu, na ni jambo limekwisha kuhukumiwa. Basi, akachukua mamba yake, na akaondoka naye mpaka mahali pa mbali, kisha uchungu ukampeleka kwenye shina la mtende, akasema: Laiti ningekufa kabla ya haya, na nikawa nimesahaulika kabisa. Mara ikamfikia sauti kutoka chini yake: Usihuzunike, hakika Mola wako ameweka kijito chini yako. Na litikise kwako shina la mtende, litakuangushia tende nzuri zilizowiva. Basi ule na unywe na uburudishe macho, na kama ukimuona mtu yoyote useme: Hakika mimi nimeweka nadhri kwa Mwingi wa rehma ya kufunga saumu, kwa hiyo leo sitasema na mtu. Kisha akampeleka kwa jamaa zake akimbeba. Wakasema: Ewe Mariam! Hakika umeleta kitu cha ajabu! Ewe dada yake Harun! Baba yako hakuwa mtu mbaya, wala mama yako hakuwa mwasherati. Ndipo akaashiria kwake, wakasema: Tutawezaje kuzungumza na mtoto wa kwenye susu? Akasema (yule mtoto) Hakika mimi ni mja wa Mwenyezi Mungu, amenipa kitabu na amenifanya kuwa Nabii. Na amenifaya mbarikiwa popote nitakapokuwa, na ameniusia swala na zaka maadamu ningali hai. Na kumfanya wema mama yangu wala hakunijaalia niwe jeuri, muovu. Na amani iko juu yangu tangu siku niliyozaliwa hadi siku nitakayokufa na siku nitakayofufuliwa na kuwa hai. Huyo ndie Isa bin Mariam, ndio kauli ya haki ambayo wanaifanya shaka.” (19:16-34).

Mariam, Yesu na Ukristo kwa Mtazamo wa Kiislam

Miongoni mwa sifa hizo zilizotajwa hapo juu, nafikri kwamba sifa mbili ni za muhimu sana na zinajumuisha hizo nyingine ndani yao, nazo ni, kuwa mwaminifu zaidi na kule kutakaswa haswa, hizi ni alama za wale watu wakamilifu.

Kwa mujibu wa Qur'an, kuna makundi manne ya watu ambayo yanakuwa juu ya mengine yote, hao ndio watu wale ambao juu yao Mwenyezi Mungu ameweka baraka zake na kila Mwislam, angalau mara kumi kwa siku ndani ya sala yake, anamuomba Mungu ili kumuongoza yeze kuelekeza kwenye njia iliyonyooka (1:6-7). Qur'an inasema: "**Na wenye kumtii Mwenyezi Mungu na Mtume, basi hao (watakuwa) pamoja na wale aliowanemesha Mwenyezi Mungu, mionganoni mwa Manabii na Masadiki na Mashahidi na watu wema, na hao ndio marafiki wema.**" (4:69)

Hivyo wale wakweli zaidi (*as-Sadiqin*) wanakuja kwenye cheo mara tu baada ya Mitume.¹⁷ Kwa hakika, kuwa wakweli zaidi ni muhimu sana kiasi kwamba wakati mwingine mitume wanasihiwa kwa kuwa wakweli zaidi.¹⁸ Ukweli hapa ni zaidi sana kuliko ukweli katika maneno ya mtu, au mazungumzo. Ukweli hapa unahitajia ukweli katika maneno, katika nia na itikadi, na katika matendo. Kwa maneno mengine, unahusisha mawasiliano na kuafikiana baina ya moyo wa mtu na akili, ulimi na vitendo.¹⁹ Mariam ndiye bibi pekee ambaye anatajwa katika Qur'an kuwa mkweli zaidi (*sidiqan*). Bila shaka, hadithi za kiislam zinatajwa wanawake wengine hususan Fatimah yule binti ya Mtume Muhammad kuwa mmoja wa wakweli zaidi.

Kuhusu utakaso, mtu lazima atambue kwamba suala zima katika safari ya kiroho ni mtu kutakasa nafsi yake. Mitume wote wamekuja kuwafundisha

¹⁷ Watu wa kila kundi huwa na sifa zote za lile kundi la chini.

¹⁸ Kwa mfano; Qur'an inasema: "Pia taja katika kitabu (habari ya) Ibrahim, yeze alikuwa mtu mkweli, na Nabii." (19:41)

¹⁹ Tazama kwa mfano Qur'an 2:177.

Mariam, Yesu na Ukristo kwa Mtazamo wa Kiislam

na kuwatakasa wanadamu.²⁰ Kwa vile Mungu ndiye Mtakatifu wa watakatifu, yejote anayetamani kumkadiria Yeye lazima ajitakase mwenyewe binafsi. Utakasaji huo ni lazima uanze kwa mtu kudhamiria mwenyewe kufuata njia ya haki, iliyonyooka. Baada ya mtu kufanya jithada kiasi iwezekanavyo na kuthibitisha dhamira halisi ya mtu ya kutakasa nafsi yake, Mungu atamuongoza na kushusha fadhila Zake kwa mja Wake huyu katika njia maalum na kumtakasa. Hivyo kuna hatua mbili: moja ni ile hatua mtu kujitakasa mwenyewe (hii ni kwa ajili ya mutatahirin na Mutaharin) na nyagine ni ile hatua ya kutakaswa na Mwenyezi Mungu (hii ni kwa ajili ya Mutahharin). Moja ya sifa ya wale waliotharishwa (*Mutahharin*) ni kwamba wao wana njia ya kufikia kwenye siri ya ufunuo mtakatifu. Kwa mfano, tunasoma katika Qur'ani:**“Bila shaka hii ni Qur’ani yenye heshima, katika kitabu kinachohifadhiwa. Hapana atakayeigusa ila waliotakaswa. Ni uteremsho utokao kwa Mola wa walimwengu.”**²¹ (56:77-80)

Ni katika maana hii kwamba Qur'ani inatuambia kuhusu utakaso wa Mariam (3:41) na utakaso wa Nyumba ya Mtume (Ahlul-Bayt) uliofanywa na Mwenyezi Mungu.²²

²⁰ Kwa mfano tazama Qur'ani 62:2

²¹ Akitoa maelezo juu ya aya hiyo hapo juu, A. Yusuf Ali anaandika hivi:

“Ni wahyi unaoelezwa na sifa nne: (1) Ni wenye kuheshimika sana, wenye ukarimu, unaodokeza, pamoja na ukweli kwamba unastahili kupewa heshima, kwamba pia unatunuku fadhila kubwa sanakwa wale wanaopokea . (2) Upo umelindika vyema, maknun, wenye thamani ndani yake binafsi na umehifadhiwa katika utakasikaji wake (3) Hakuna atakayekigusa ila waliotakasika, wasafi katika mwili, akili, fikra, dhamiri na nafsi; ni watu kama hao tu watakaopata uhusiano halisi nacho na maana yake kamili. (4) Ni wahyi au ufunuo unaotoka kwa Mola wa walimwengu, na kwa hiyo ni wa jumla kwa watu wote.

²² “**Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu watu wa nyumba (ya Mtume) na kukutakaseni utakaso wa sawasawa.**” (33:33).

Mariam, Yesu na Ukristo kwa Mtazamo wa Kiislam

Sasa hebu turejee kwa ufupi kwenye baadhi ya vipengele vya mtazamo wa Kiislaam kuhusu Yesu.

YESU (ISA)

Yesu anatajwa ndani ya Qur'ani kwa zaidi ya Mara tisini, na kuna maelezo mengi katika hadithi za Kiislam juu ya Yesu, pamoja na simulizi zake na tabia yake.²³ ²⁴ Tayari tumekwishaelezea kuzaliwa kwake kwa njia ya bikira na kwamba alikuwa mmojawapo wa wale mitume watano mashuhuri amba wanajulikana kama “*Ulu al-'Adhm*” yenye maana ya wenyе dhamira kubwa. Kwa kawaida inaaminiwa kwamba wote hao watano walikuwa na ujumbe wa kimataifa.²⁵ Kuwa mtume, na hasa, kuwa mmoja wa wale mitume wakubwa kabisa kunaonesha kuwa na sifa za hali ya juu kabisa kama vile kutokuwa na dhambi, kutoharika na pia kutokosea.²⁶ Sio tu kwamba kuzaliwa kwake kulikuwa kwa muujiza kama ishara ya kudura za Mwenyezi Mungu, bali pia utoto au uchanga wake. Alikuwa na uwezo wa kuongea alipozaliwa tu.²⁷

²³ Yesu anatajwa katika Qur'ani kwa namna tofauti, wakati mwngine kwa jina lake hasa na wakati mwngine kwa vyeo au sifa kwa mfano, neno Isa (Yesu limetajwa mara 25, Masihi mara 11, na mwana wa Mariam mara 33, Nabii (Mtume) mara moja, Rasuli (Mjumbe) mara tatu.

²⁴ Kwa mfano kuhusu Isa (Yesu) na maisha yake ya kawaida tazama *Nahajul-Balaghah*, hotuba namba 159, uk. 324.

²⁵ Kwa mfano, Sayyid M.H. Tabataba'i anaandika: “Kwa hakika, Isa (Yesu) alikuwa mmoja wa *Ulu al-Adhim* kama Musa na walitumwa kwa watu wote wa dunia nzima.” (*Tabataba'i* Juz. 3, uk. 218)

²⁶ Kwa mujibu wa itikadi ya Shi'ah, uma'sum au kutokukosea kwa mitume kunahuishisha kazi zao za utume na katika maisha yao binafsi.

²⁷ Tunarejea kwenye tanbihi ya 16 kwenye aya za Sura ya 19 zinazoashiria maneno yake halisi kama kichanga kilichozaliwa punde tu.

Mariam, Yesu na Ukristo kwa Mtazamo wa Kiislam

“Atasema na watu katika uchanga wake na utu uzima wake, na atakuwa katika watu wema.” (3:46)

Katika muda wa ujumbe wake, Yesu alikuwa na uwezo wa kufanya miujiza kama ishara ya ukweli wa ujumbe wake na alisimamiwa kimsaada na Mwenyezi Mungu. Qur’ani inarejea kwenye jambo hilo ndani ya aya kadhaa kama vile”“(Kumbuka) wanafunzi (wake) waliposema: ‘Ewe Isa mwana wa Mariam je, Mola Wako anaweza kututeremshia chakula kutoka mbinguni.? Akasema (Nabii Isa), ‘Mcheni Mungu ikiwa ni wenye kuamini.’ Wakasema: ‘Tunataka kukila chakula hicho na nyoyo zenu zitulie na tujue kwamba umetwambia kweli na tuwe miongoni mwa wanaoyashuhudia.’”

“Akasema Isa Ibn Mariam: Ewe Mwenyezi Mungu! Mola wangu! Tuteremshie chakula kutoka mbinguni ili kiwe siku kuu kwa ajili ya wa mwanzo wetu na wa mwisho wetu, na kiwe dalili itokayo Kwako, na uturuzuku, na wewe ni Mbora wa wanaoruzuku.”

“Mwenyezi Mungu akasema: “Bila shaka Mimi nitateremsha juu yenu, lakini mionganini mwenu atakayekataa baada ya haya, basi Mimi nitamuadhibu adhabu ambayo Mimi sijamuadhibu yoyote katika walimwengu.” (5:112-115)

Mahali pengine Qur’ani inarejelea kwenye miujiza mingine ya Yesu:

“.....Hakika mimi nimewajieni na dalili itokayo kwa Mola wenu. Mimi nitakufanyieni katika udongo kama namna ya ndege, kisha napuliza ndani yake (awe) ndege kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Na niwapoze vipofu na wenye mbaranga, niwafufue wafu kwa idhini ya Mwenyezi Mungu.....” (3:49)

“....Ewe Isa mwana wa Mariam! Kumbuka neema Yangu juu yako, na juu ya mama yako, nilipokutia nguvu kwa roho takatifu,

Mariam, Yesu na Ukristo kwa Mtazamo wa Kiislam

ukazungumza na watu katika utoto na utu uzima. Na nilipoku-fundisha kitabu na hekima na Tourati na Injili. Na ulipotengeneza kutokana na udongo sura ya ndege kwa idhini yangu, na ukapuliza ndani yake na akawa ndege (kamili) kwa idhini yangu. Na uli-waponyesha vipofu na wakoma kwa idhini yangu, na ulipowafufua wafu kwa idhini yangu na nilipokukinga na wana wa Israili ulipowa-jia na hoja zilizo wazi na wakasema waliokufuru mionganoni mwao: “Haya si lolote ila ni uchawi mtupu.” (5:110)

Yesu alikuwa ni Masihi aliyeahidiwa:“(Kumbukeni) Malaika walipose-ma: “Ewe Mariam! Hakika Mwenyezi Mungu anakupa habari njema za neno litokalo Kwake, jina lake ni Masihi Isa mwana wa Mariam, mwenye heshima ulimwenguni na Akhera, na ni mionganoni mwa wenye kukurubishwa mbele ya Mwenyezi Mungu.” (3:45)

Aya hiyo hapo juu inaonyesha kwamba Yesu alikuwa “Neno la Mungu,” lenye heshima katika ulimwengu huu na ule wa Akhera, na mionganoni mwa wale waliosogezwa karibu na Mwenyezi Mungu (*Muqarrabin*). Kwa vile njia pekee ya kuwa karibu na Mungu ni kumuabudu na kumtumikia Yeye kwa kweli, Yesu alikuwa “Mtumishi wa Mungu” wa kweli (*Abdullah*) (19:30), “Aliyebarikiwa” au “chanzo cha baraka” (*Mubarak*) (19:31), na “Maneno ya haki” (*Qaul al-Haqq*) (19:34). Katika aya 4:171, Yesu anaelezwa kama “Nabii wa Mungu,” “Neno” ambalo yeye amelitoa kwa Mariam na “Roho (itokayo) kutoka Kwake” (*Ruhan Minhu*). Yesu vile vile alipewa dalili za wazi na “alisaidiwa na Roho Mtakatifu.” (2:253)

UHUSIANO WA WAISLAM NA WAKRISTO

Baada ya kurejea baadhi ya vipengele vya shaksia za Mariam na Yesu, sasa ni wakati wa kuzungumzia uhusiano wa Wakristo na Waislam. Kuna njia mbali mbali za kuweza kushughulika na suala hili muhimu linaloongeze-ka. Katika yafuatayo, ningependa kulizungumzia jambo hili kwa njia ya mzunguko, isiyo ya moja kwa moja, yaani kwamba, kwa kuelezea kile nili-

Mariam, Yesu na Ukristo kwa Mtazamo wa Kiislam

chokuwa nikiwaambia rafiki zangu wa Kikristo mara kwa mara, kwamba mimi kama Muislam, huwa ninafarijika na kufurahia na mazungumzo na mshikamano baina ya Waislam na Wakristo. Sababu ya kauli kama hiyo imetegemea katika mambo yafuatayo:

Wote tunamuamini na kumuabudu Mungu yule yule ambaye ni Mmoja, Mwingi wa Rehma, Mkarimu, Mwenye Enzi, Mwenye Maarifa, Mwenye kuenea pote. Waislam na Wakristo wote wanampenda sana Mungu na wanajaribu kumcha na kumyenyekaa na kujikurubisha Kwake. Tunasoma katika Zaburi 42:2 “Moyo wangu una kiu kwa ajili ya Mungu, Mungu wa uhai; lini nitakapokwenda kuutafuta Uso wa Mungu?” Na katika Qur’ani:

“Na Mashariki na Magharibi ni ya Mwenyezi Mungu; basi popote mtakakogeukia ndipo uliko uso wa Mwenyezi Mungu.....” (2:115) kuna hali ya kiroho kubwa na muhimu sana yenye kufanana katika dini zote hizi.

Sisi sote tunaamini katika uhuru kamili wa dhamira ya binadamu na wajibu wake na uwajibikaji wake mbele ya Mwenyezi Mungu na tunachangia uelewa mmoja juu ya maadili makuu ya msingi.²⁸

Sisi sote tunaamini juu ya ufufuo na ushuhulikiwaji wa watu na Mwenyezi Mungu kwa haki na huruma au neema katika siku ya Kiyama.

Sote tuna taadhima kubwa ya zawadi ya akili na dhamiri na wakati huohuo

²⁸ Tunadhani kwamba watu wote, lakini hususan hasa Waislam, wanaweza kushirikiana nasi yale madili tuliyoyapata kutoka kwa Isa (Yesu): Utii kamili kwenye utashi wa Mwenyezi Mungu ushahidi uliotolewa kwenye haki na kweli unyenyekevu katika tabia, udhibiti wa maneno yake mtu, uadilifu katika vtendo vyake mtu, huruma inayoonyeshwa katika vitendo, upendo kwa wote, msamaha unaotolewa kwa makosa yaliyotendeka, kudumisha amani pamoja na ndugu wote akinadada na kaka.” Kadinali Francis Arinze, Ujumbe kwa Waislam kwa ajili ya mwisho wa mfungo wa Ramadhani,2000.

Mariam, Yesu na Ukristo kwa Mtazamo wa Kiislam

tunatambua haja yetu juu ya ufunuo wa ki-mbinguni katika njia yetu kuelekea kwenye furaha katika dunia hii na ile ijayo ya Akhera.

Sote tunaamini kwamba wanadamu wote wanatokana na baba yule yule na mama, yaani Adam na Hawa. Tunayo hisia kubwa za urafiki na tunakataa aina yoyote ile ya ubaguzi.²⁹ Tunaamini katika heshima ya mwanadamu na kupinga vitendo vyovyyote vyta kidhalimu nya wanadamu.³⁰ Tunaitambua thamani ya maisha au uhai wa mwanadamu kama zawadi kubwa ya kimungu.

Wote tunaamini katika Utume na tunachangia historia ndefu ya unabii huu tangu mwanzoni kabisa mwa historia ya Mwanadamu.

wote tunayo heshma kubwa sana kwa Nabii Ibrahim (a.s) na tunamchukulia kama mfano wa wajibu na kwa hakika kama “Baba wa Waumini wote.”

Wote tunayo heshima kuu na upendo juu ya Mariam na mwanawe Yesu, amani iwe juu yao wote. Tunaamini katika kuzaliwa kwake katika njia ya ubikira na tunangojea kurejea kwake kwa mara ya pili.

Tunachangia wote uhusiano mkubwa kuhusu changamoto ya kuishi maisha ya kidini leo hii, kunakosababishwa na utamaduni wa leo wa uyakinifu na

²⁹ “Hii ina maana kwamba dini ni adui wa utengano na ubaguzi, wa chuki na uadui, wa vurugu na migogoro.” (Papa John Paulo II, kwa viongozi wa kikristo, Wayahudi na Waislam, Jerusalem 23 Machi 2000) Tazama pia *Katekasimo* ya kanisa Katoliki namba: 842

³⁰ Dr George Carey, Askofu Mkuu wa Canterbury: Si katika yoyote kati ya dini na imani zetu ambamo Mungu ni kitu cha udadisi wa kielimu wa bure bure tu. Tunashuhulika na Mungu aliye hai, Mwenye upendo, uumbaji Wake kwenye ukamilifu unaofaa, na jamii ya mwanadamu kuishi pamoja kwa haki na amani. Ni Mungu huyu ambaye mwongozo Wake tunautafuta na ambaye tunatumikia utukufu Wake. (*The Road Ahead: A Christian Muslim Diloque*, uk. x)

Mariam, Yesu na Ukristo kwa Mtazamo wa Kiislam

maoni ya kwamba dini isiwe msingi wa elimu ya maadili.³¹

Ninaamini katika upatanifu wa ufunuo wote (wa manabii) na utume wote. Hapajawahi kuwa na ushindani au uadui baina ya Mitume au kati ya wafuasi wao wa kweli. Kwa kweli Uislam, ambao kwa asili ni ule unyenyekefu wote kwa Mungu, ndio dini ya Mitume wote. Mtume Muhammad aliwathibitisha Mitume wote waliotangulia ikiwa ni pamoja na Yesu, na yeze mwenyewe alikuwa ametabiriwa nao.

Mimi, kama Muislam, sina haja ya kumkana Yesu au ujumbe wake. Kwa kweli, kuwa mwaminifu kwa dini yangu hasa, ni lazima niamini Mitume wote na funuo zao. Qur'ani inamtaka Muislam kutamka imani yake katika Mitume waliotangulia na ufunuo wao.

Sema: “Tumemwanini Mwenyezi Mungu na yale tuliyoteremshiwa, na yaliyoteremshwa kwa Ibrahim na Ismail na Yaqub na Makabila na alichopewa Musa na Isa na Manabii kutoka kwa Mola wao. Hatubagui

³¹ “Wao (Wakristo) ni lazima waangalie ubadilikaji mkubwa ambao unatokea mionganini mwa mataifa na kufanya kazi kwa bidii ili kwamba mwanadamu wa kisasa hageuzwi mbali na mambo ya Mungu kwa ushughulishwaji zaidi na sayansi na teknolojia ya kisasa.” (Baraza la pili la Vatican, Agizo juu ya kazi za kimisionari za Kanisa. Ad Gentes, Desemba, 1965, nn 11,13.

“Kama waumini, hatukatai au kutupilia mbali yoyote kati ya faida halisi ambayo maendeleo ya kisasa yameleta, bali tunathibitisha hata hivyo kwamba bila kurejea kwa Mungu, sayansi ya kisasa haiwezi kumuongoza mwanadamu, mwanaume na mwanamke kwenye lengo ambalo wameumbiwa. Ni hapa vile vile ambapo Wakristo na Waislam wanaweza kufanya kazi pamoja kushuhudilia mbele ya ustaarabu wa kisasa juu ya utukufu uliopo na majaliwa ambayo yanaongoza hatua zetu. Wote kwa pamoja tunaweza kutangaza kwa kutamka kwamba yule aliyetumba sisi ametutaka tuishi kwa upatanifu na amani na uadilifu. Baraka za Yule Aliye juu kabisa ziwe pamoja nanyi katika jitihada zenu juu ya mjadala na amani.” (Papa John Paul II, kwa ujumbe wa Jumuiya ya wito wa Kiislam wa dunia 15 January 1990).

Mariam, Yesu na Ukristo kwa Mtazamo wa Kiislam

baina yao hata mmoja, na sisi ni wenyenyekeea Yeye” (3:84)

Kwangu mimi, hakuna haja ya kukana au kuficha zawadi za Yesu au sifa zinazofaa za Ukristo. Hizi zote ni ishara za Ukuu wa Mungu yule yule. Hizi zote ni neema za kiungu ambazo zinaongeza utajiri wangu, ambao kwa huo ni lazima niwe mwenye shukurani sana.

Sina haja ya kuafikiana kuhusu itikadi yangu ili kuingia kwenye mjadala halisi, endelevu na wenyenyekeea pamoja na wakristo. Kwa kweli, ni Qur’ani yenye ambayo inaitisha mjadala kama huo pamoja na wafuasi wote wa itikati ya Ki-Ibrahim. Hivyo kwangu mimi, kuingia kwenye mjadala kama huo na kujenga mambo ya kawaida (kwa wote) kuna mizizi ndani ya Qur’ani, na sio mtindo tu au urasimu kikanuni.

Qur’ani inaonyesha upendo mkubwa juu ya Wakristo kwa sababu ya unyenyeketu wao, kutafuta kwao ukweli na utu wema wao kwa Waislam. Kwa mfano, tunasoma ndani ya Qur’ani hivi:“.....**Na utawaona walio karibu zaidi kwa mapenzi na waumini ni wale wanaosema: ‘Sisi ni Wakristo.’** Hayo ni kwa sababu wako mionganoni mwao wanachuoni na wamchao **Mwenyezi Mungu na kwamba wao kawatacabari. Na wana-** posikia yaliyoteremshwa kwa Mtume, utaona macho yakichuruzika machozi kwa sababu ya haki waliyotambua

” (5:82-83)

Kwa kutumia uhusiano wangu wa karibu na endelevu pamoja na wakristo wengi nimefikia uamuzi wa mwisho kwamba maelezo ya Qur’ani na sifa za Wakristo wa wakati wa Mtume Muhammad zinaweza kushuhudiwa katika nchi za kikristo leo hi. Wapo Wakristo waaminifu, watafuta kweli, wanyenyeketu na wenyenyekeea na mioyo mizuri ambao wameyatoa maisha yao kwa Mungu na sioni sababu kwa nini mimi nisiwachukulie watu hawa kama wawakilishi wa kweli wa Ukristo, badala ya wale wanaodai utengano, uadui na ugomvi mionganoni mwa waumini na wako mbali na kutekeleza ile amri ya upendo. Kwa bahati mbaya leo hii ni rahisi kudanganywa. Kuna watu wanaoitwa “Waislam” au “Wayahudi” au “Wakristo” lakini kwa

Mariam, Yesu na Ukristo kwa Mtazamo wa Kiislam

namna yoyote ile mtu hawazi kuamua kuhusu imani zao kwa kuzingalia tabia zao. Na hii inakuwa mbaya zaidi endapo kuna jaribio la makusudi la kuwasilisha vibaya maisha ya imani kwa jumla na kwa dini fulani halisi.

Inanisaidia sana mimi kuona kwamba washirika katika majadiliano wanarudisha yale mapenzi na heshima ambayo mimi ninayo kwa ajili yao na imani zao za kidini. Hapa ningependa kurejea kwa ufupi kwenye uelewa wa kikristo juu ya Uislam na kutoka mfano kwenye uelewa wa Kikristo juu ya Uislam na kutolea mfano ukweli kwamba mahusiano haya ya heshima na mapenzi tayari yamekwisha anzishwa.³² kwa vile kazi hii

³² Ni kweli kwamba kumekuwa na nyakati za huzuni katika historia ya makabiliano baina ya Wakristo na Waislam. Hata hivyo kumekuwa na masuala mengi ya maisha ya heshima kwa pamoja vile vile. Kwa bahati mbaya upande huu wa sarafu unaonekana kwa nadra sana. Kwa mfano, mwanzoni kabisa mwa Uislam, Waislam waliokuwa wamehamia Ethiopia waliungwa mkono na Najjashi, mfalme wa Kikristo. Mwanachama mmoja wa chama cha kikristo wa huko Canada, Ovey N. Mohammed anaandika hivi: “Kufuatana na mfano wa Muhammad katika kushughulika na Wakristo wa Najran na Mafundisho ya Qur’ani kwamba ‘Hakuna kulazimishana katika dini’ (Qur’ani 2:256), Wakristo waliruhusiwa kubakia katika nchi ya Kiislam kuitia kufanya mikataba na mamlaka za Kiislam. Wengi walichagua kufanya hivyo badala ya kuhamia kwenye nchi za Kikristo ambako mateso kwa kisingizio cha imani halisi yalienea.” (uk.32) Baadaye pia anaongeza: “Inapaswa ifahamike kwamba kabla ya kuinukia kwa ukoloni, Wakristo waliokuwa wakiishi katika nchi za Kiislam walifaidika kwa jumla na kiwango cha kuvumiliana, mfano ambao hauwezi kupatikana huko Ulaya hadi kwenye nyakati za kisasa kabisa.” (uk 41)

Mariam, Yesu na Ukristo kwa Mtazamo wa Kiislam

inahusika hasahasa na majadiliano baina ya Uislam wa Shiah na Roman Catholic, nitarejelea. Hapa chini kwenye vyanzo vya Ki-Katoliki.³³

³³ Imeonyeshwa na waandishi wengi kwamba kwa nyongeza juu ya kufanana kwa kawaida kati ya Uislam na Ukristo kuna kufanana kwingi zaidi kati ya Ushi'a na Ukatoliki wa Kiroma. Kwa mfano, tazama Makala ya James A. Bill na John Alden Williams, "Uislam wa Shi'a na Ukatoliki wa Kiroma: Uchambuzi wa kidini na kisiasa," katika *The Vatican, Islam, and the Middle East*, kilichohaririwa na Kail C. Ellis (Syracuse, N.Y. Syracuse University Press, 1987) na Overy N. Mohammed, *S.J. Muslim Christian Relations: Past, Present, Future* (New York: Orbis Books 1999). Miongoni mwa yanayofanana; yafuatayo yanaweza kuorod-heshwa:

- Mfumo wa ngazi za kidini wa Shi'ah una yaliyo sambamba nayo katika Ukatoliki
- Msisitizo juu ya dhana ya "Mateso" na kufanana kati ya kifo cha Imam Husein na Yesu. Bill na Williams wanasisistiza: "Katika kadhia zote, mfululizo wa matukio ya mateso na hekaya za mateso au kifo cha kishahidi vimerasimishwa na kubakia kuwa sehemu hai na muhimu za mfumo wa Imani."
- Kufanana kwa shaksia ya Mariam na Fatimah binti ya Mtume Muhammad kama kielelezo cha mama mwenye huzuni katika moyo wa familia tukufu.
- "Umuhimu wa vitendo vya kimujiza."
- "Utambuzi wa mfumo wa kisheria wenye msingi wake juu ya kauli ambayo mamlaka yote yanatoka kwa Mungu."
- "Kinyambuo kwa ajili ya kuanzisha mifumo ya kijamii na kisiasa ambayo itazalisha au kulea Uadilfu, uhuru na Usalama."

Katika kitabu cha hivi karibuni, Bill na Williams wanaandika: "Wachache katika ulimwengu wa Magharibi wanavielewa vile viunganisho vingi vya kusismua kati ya Ushi'ah na Ukatoliki. Kwa mfano, katika Qur'an, Yesu anatajwa ndani ya aya zaidi ya tisini. Kuna utajo mwangi juu ya Mariam ndani ya Qur'an zaidi kuliko ndani ya Biblia; kwa kweli, Mariam anatajwa sana zaidi kuliko Mwanamke yoyote. Kuna Maimamu kumi na mbili, viongozi walioteuliwa na Mungu kulingana na imani za Kishi'ah na mitume kumi na mbili (wanafunzi wa Yesu) katika Ukristo, Maimam kumi na moja wa kwanza wanaaminiwa kuwa wamekuwa kama Mashahidi na isipokuwa kwa Yuda Iskariote na Mtakatifu Yohana, hao wanafunzi wa Yesu pia walielezewa kuwa waliuawa mashahidi. La kushangaza zaidi, tarakimu 72 inajitokeza mara kwa mara katika simulizi au mila zote....."

(*Roman Catholics and Shi'i Muslims: Prayer, Passion and Politics*, [Chapel Hill: University of North Carolina], (uk.3)

Mariam, Yesu na Ukristo kwa Mtazamo wa Kiislam

A. KUWA TAYARI KWA MJADALA NA USHIRIKIANO NA WAISLAM

Umekuwepo uwazi katika katika Kanisa kwa jumla na hususani katika Kanisa la kikatoliki, la Roman baada ya lile Baraza la II la Vatican kwa dini za wasiokuwa Wakristo, hasa zile dini zenye asili ya ki-Abraham.³⁴ Majaribio mengi sana yamefanywa husuan katika miongo michache iliyopita, kwa ajili ya mjadala wenyewe manufaa baina ya Waislam na Wakristo ili kufikia kuelewana kwa pamoja na ili kujenga madaraja baina ya makundi mawili hayo kwa ajili ya kufanya kazi pamoja na kuzimudu changamoto zinazotishia jumuiya yote ya kidini pamoja. Juu ya umuhimu wa mjadala huu, Papa Yohana Paulo II anasema:

“Kanisa Katoliki linapenda kuendelea na mjadala wa dini mbili wa ukweli na uaminifu wenyewe kuzaa matunda pamoja na wafuasi wa Uyahudi na Uislam. Mjadala kama huo sio jaribio la kulazimisha maoni yetu juu ya wengine, kile unachokitaka mjadala huu kwetu sote ni kwamba, tukiwa tumeshikilia kile tunachoamini, tuwe tunasikilizana na kila mmoja wetu kwa heshima kutafuta kutambua yote yale ambayo ni mazuri na matakatifu katika mafundisho ya kila mmoja wetu, na kushirikiana katika kuunga mkono kila kitu kinachopendelea maelewano ya pamoja na amani. (*Pope John Paul II To Christian, Jewish and Muslim Leaders*, Jerusalem, 23 March, 2000) – [Papa John Paulo II kwa viongozi wa Wakristo, Wayahudi na Waislam, Jerusalem, 23 Mchi, 2000]

B. HESHIMA KUBWA KWA AJILI YA WAISLAM:

Juu ya heshima na taadhima ya Kanisa kwa ajili ya Waislam, mtu anawaza kurejea kwenye nyaraka zifuatazo:
Kanisa linawaangalia kwa heshima kuu Waislam vile vile. Wao

34. Kwa mfano, Papa John Paul II katika nafasi ya Uislam katika mjadala huu anasema: “Katika mjadala huu, Wayahudi na Waislam wanapaswa kuwa na nafasi nzuri zaidi. (Pope John Paul II, Apostolic letter on Preparation for the Jubilee 2000 Tertio Millennio Adveniente, 10 November, 1994, n 52)

Mariam, Yesu na Ukristo kwa Mtazamo wa Kiislam

wanamuabudu yule Mungu Mmoja, aliye Hai na anayejitosheleza mwenyewe; Mwingi wa Rehema, Mwenye nguvu, Muumba wa mbingu na ardhi (5) ambaye amezungumza na watu; wao wanafanya kila jitihada kukubali kwa moyo mmoja hata amri Zake zenye mafumbo magumu kueleweka, kama vile Abraham, ambaye kwaye itikadi za Kiislam zinafurahia kuihusisha dini hiyo naye, alivyojisalimisha kwa Mungu Wake. Ingawa hawamkubali Yesu kama Mungu, wanamtukuza yeye kama Nabii. Vile vile wao wanamheshima Mariam, mama yake Bikra, wakati mwininge wanamtaja kwa moyo wa upendo kabisa. Aidha wanaingojea Siku ya Hukumu ambapo Mungu atawapa wale wote waliofufuliwa kutoka kwa wafu, yale waliyokuwa wameyaacha nyuma (amali zao) mwisho kabisa, wao wanathamini maadili ya maisha na wanamuabudu Mungu husasan kwa njia ya Swala, kutoa Sadaka na kufunga. (*NOSTRA AETATE*)

C. KUUTAMBUA WOKOVU WA WAISLAM:

Kanisa linaamini kwamba hakuna ukiritimba juu ya wokovu, Mpango wa wokovu vile vile unawaingiza wale ambao wanamkubali Muumba, kwanza kabisa mionganii mwao ambao ni Waislam, hawa wanatangaza kufuata dini ya Abraham, na pamoja na sisi wanamuabudu yule Mungu mmoja Mwingi wa neema, Hakimu wa wanadamu Siku ya Mwisho. (*Katekismo ya kanisa Katoliki Na: 841* kutoka Luman Gention Na:16)

D . KUUTAMBUA UISLAM KAMA DINI NDUGU; WAISLAM KAMA NDUGU – MADADA NA KAKA KATIKA IMANI:

Sio tu kwamba kanisa linakubali wokovu wa Waislam, bali pia linauchukulia Uislam kama kielelezo halisi cha imani ya Ibrahim:

“Wanayo kama ninyi, amani ya Ibrahim katika Mungu Mmoja, Mwenye enzi na Mungu Mwenye Neema. (Papa John Paulo II kwa jumuiya ya Wakatoliki wa Ankara, 3 Desemba, 1979)

Mariam, Yesu na Ukristo kwa Mtazamo wa Kiislam

Mungu wenu na Mungu wetu ni mmoja, na sisi ni ndugu, dada na kaka katika imani ya Ibrahim. (Papa John Paulo II kwa vijana wa Kiislam wa Morocco, Casablanca, 19 Augusti 1985)

E. HESHIMA JUU YA MTUME MUHAMMAD:

Kwa kawaida heshima ya Kanisa kwa Uislam haiishii kwa wafuasi wake tu, yaani Waislam. Inaendelea pia hadi kwa Mtume Muhammad na maadili aliyoyafundisha. Kama Kadinali Tarancon, ambaye ni Raisi wa Baraza la Maaskofu la Hispania alivyoliweka kwenye Mkutano wa kimataifa wa Waislam na Wakristo huko Cordoba mwaka 1977:

“Itawezekana vipi kuutambua na kuuthamini Uislam na Waislam bila kuonyesha thamani kwa Mtume wa Uislam na maadili aliyoyatangaza na kuyasimamia? Kutokufanya hivyo hakutakuwa kukosa heshima tu ambayo Baraza (la Vatican) linawasihi Wakristo, lakini pia ni kupuuza kipengele cha kidini ambacho fikira lazima ichukuliwe katika tafakari ya kitheologia na utambuzi makini wa kidini.³⁵

³⁵ Katika hotuba ile, Kadinali Tarancon aliwataka Wakristo, kama alivyofanya Askofu Timothy wa Baghdad (aliyekufa mwaka 823) kwamba “Muhammad alipita katika njia ya Mitume.” (Imenukuliwa katika ‘Muhammad’ uk.64). .Inapendeza sana kuona kwamba kuna wakristo waaminifu wengi sana ambao kwa mafundisho ya Paulo kwamba watakuwepo mitume wakweli baada ya Yesu (‘Wakarintho 14:29,39;12:10,28; Warumi 12:6) wanamtambua Muhammad kama Mtume halisi. Kwa orodha ya mfano ya wanafikra wa kikatoliki na kiprotestanti ambao wameandka kwa kumuunga mkono katika wazo hili Taz: Mohammed. Uk. 119, maelezo ya 65 na 66).J.M Gashell katika kitabu chake ‘Explaining Islam: Islam from a Catholic Perspective uk.29, anaandika: “ Wakristo wengi wanajaribu kufikiri juu ya Mitume kimsingi kama Agano la Kale linavyoonyesha kwa mpokezano kutaja tahadhari zenyetutu na kuahidi zama za amani za kimasih, na kuupuza ukweli kwamba zawadi ya Utume ni moja ya Zawadi za yule Roho zilizoorodhesawa na Mtakatifu Paulo.....”

Mariam, Yesu na Ukristo kwa Mtazamo wa Kiislam

Nadhani sasa iko wazi kwamba Wakristo na Waislam wako karibu sana na kila mmoja wao; wanachangia mengi na hakuna sababu kwa nini kusiwe na hisia nzito ya umoja kati yao. Kwa kweli kama ulivyoona hapo juu, kuna sababu nyingi zinazowataka kuwa pamoja na kufanya kazi pamoja kwa maendeleo ya wanadamu.

Bibliografia:

* Aguis, Alfred (2002) *Interfaith Dialogue: The Teachings of the Catholic Church*, Mkutano wa maaskofu wa katoliki wa Uingereza na Wales.

* Al- Kulayni, Muhammad Ibn Ya'qub (1984), *Usul al-Kafi* (Tehran: Dar al- Kutub al Islamiyyah, Chapa ya Tano)

* Arinze Francis (2000) *Meetings in Friendship: Messages to Muslims for the End of Ramadhan* (1967-2000) (Vatican City: Baraza la ki-Papa kwa ajili ya Majadiliano baina ya dini mbali mbali)

* Bahmanpour, Muhammad J. (2001), *Mary in Islam* (London: Spring)

* Gaskell, J. M. (2003), *Explaining Islam: Islam from a Catholic Perspective* (London: Jumuiya ya Ukweli wa Katoliki)

* Ipgrave, Michael (2002) *The Road Ahead: a Christian Muslim Dialogue* (London Church House Publishing)

* James A. Bill and John Alden Williams (1987), “Uislam wa ki-Shi'i na Ukatoliki wa Roman: Uchambuzi wa ki-Kanisa na kisiasa,” katika *The Vatican, Islam and Middle East*, kilichohaririwa na Kail C. Ellis (Syracuse, N.Y. Syracuse University, Press)

* James A. Bill na John Alden Williams (2002), *Roman Catholics and Shi'i*

Mariam, Yesu na Ukristo kwa Mtazamo wa Kiislam

Muslims: Prayer, Passion & Politics (Chapel Hill: University of North Carolina)

* Heydarpoor, Mahnaz (2002) *Love in Christianity and Islam* (London: New City).

* Makarim Shirazi, Nasir (2001) *Qesseha-ye Qur'an* (Tehran: Dar al-Kutub al-Islamiyyah).

* Ovey N. Mohammed, S.J. (1999), *Muslim-Christian Relations: Past, Present, Future* (New York: Orbis Books).

* Shomali Mohammed Ali (2003), *Discovering Shi'i Islam*, (Qum: Jami'at al-Zahra, Toleo la Pili.

* Tabataba'i, Sayyid Muhammad Husayn (1972) *Al-Mizan fi Tafsir al-Qur'an, Jz. 14*, (Qum: Isma'iliyan)

* *Catechism of the Catholic Church*, (1999), Revised edition, (London: Geoffrey Chapman).

Mariam, Yesu na Ukristo kwa Mtazamo wa Kiislam

ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL - ITRAH FOUNDATION:

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuu ya kwanza mpaka Ishirini
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhangga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudharr
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi

Mariam, Yesu na Ukristo kwa Mtazamo wa Kiislam

25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu
27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an.
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua Indal Ahlul Bayt
33. Udhuu kwa mujibu wa Kitabu na Sunna.
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyeezi Mungu na sifa zake
36. Amateka Na Aba' Khalifa
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana.
39. Upendo katika Ukristo na Uislamu
40. Nyuma yaho naje kuyoboka
41. Amavu n'amavuko by'ubushiya
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya swala mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipyta
46. Kusujudu juu ya udongo
47. Kusheherekea Maulidi Ya Mtume (s)
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza Swala safarini
51. Kufungua safarini
52. Umaasumu wa Manabii
53. Qur'an inatoa changamoto

Mariam, Yesu na Ukristo kwa Mtazamo wa Kiislam

54. as-Salaatu Khayrun Mina -'n Nawm
55. Uadilifu wa Masahaba
56. Dua e Kumayl
57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu
58. Umaasumu wa Mitume - Faida Zake Na Lengo Lake
59. Umaasumu wa Mitume - Majibu Ya Aya Zenye Utata
60. Umaasumu wa Mitume - Umaasumu wa Mitume Muhammad (s)
61. Nahju'l-Balaghah - Juzu ya Kwanza
62. Nahju'l-Balaghah - Juzu ya Pili
63. Kuzuru Makaburi
64. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tatu
67. Tujifunze Misingi Ya Dini
68. Sala ni Nguzo ya Dini
69. Mikesha Ya Peshawar
70. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
71. Ubora wa Imam 'Ali Juu ya Maswahaba Na Ushia ndio njia iliyonyooka
72. Shia asema haya, Sunni asema haya, Wewe wasemaje?
73. Liqaa-u-lлаah
74. Muhammad (s) Mtume wa Allah
75. Amani na Jihadi Katika Uislamu
76. Uislamu Ulienea Vipi?
77. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)
78. Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)
79. Nahjul Balagha Sehemu ya Kwanza
80. Nahjul Balagha Sehemu ya Pili
81. Ujumbe

Mariam, Yesu na Ukristo kwa Mtazamo wa Kiislam

BACK COVER

Waislamu wanaamini kwamba idadi ya Mitume wote waliotumwa na Mwenyezi Mungu ni zaidi ya 124,000 - wa kwanza wao ni Adam (a.s.) na wa mwisho wao ni Muhammad (s.a.w.). Miongoni mwa Mitume hao, wako amba Mwenyezi Mungu amewatukuza zaidi kuliko wengine, akiwemo Isa (Yesu) bin Maryam (Mariamu): "*Mitume hao tumewafadhilisha baadhi yao zaidi kuliko wengine. Miongoni mwao yuko ambaye Mwenyezi Mungu alisema naye; na wengine akawapandisha vyeo, na tukampa Isa mwana wa Maryam dalili zilizo wazi na tukamtia nguvu kwa roho takatifu...*" (Qur'an 2:253)

Ingawa Mitume wote kazi yao ilikuwa ni kufikisha ujumbe kwa wanadamu, lakini wao ni kama walimu amba kazi yao ni kufundisha, isipokuwa tu hutofautiana katika ufundishaji, k.v. wako wanaofundisha shule za msingi amba hawalingani na wanaofundisha shule za sekondari na amba hawalingani na wanaofundisha katika vyuo vikuu. Lakini pamoa na kutolingana huko, wote kazi yao ni kufundisha - ni walimu: "*Mitume ameamin yaliyoteremshwa kwake kutoka kwa Mola wake, na wenye kuamini, wote wamemwamini Mwenyezezi Mungu, na Malaika Wake, na Vitabu Vyake, na Mitume Yake, (husema): 'Hatutofautishi baina ya Mitume Wake' ...*" (Qur'an 2: 285).

Katiko moyo huu, kijitabu hiki kimeandikwa. Juhudi zimefanywa kuwasilisha kwa mukhtasari na kwa usahihi picha ya Mariamu na Isa (Yesu) katika Qur'an na kueleza kwanini ni muhimu kwa Waislamu na Wakristo kushiriki katika mazungumzo ya kweli na yenye manufaa.

Kimetolewa na kuchapishwa na:

Alitrah Foundation

P.O. Box 19701 Dar es Salaam, Tanzania

Simu:+255 22 2110640

Simu/Fax: +255 22 2127555

Email: alitrah@raha.com

Website: www.alitrah.org

Online: www.alitrah.info



Mariam, Yesu na Ukristo kwa Mtazamo wa Kiislam
